Sera, Mikakati Safi… Lakini Walengwa Je?

Policies, Programs Good… but what about the People?



Sera, Mikakati Safi…

Lakini Walengwa Je?

Policies, Programs Good…
but what about the People?



Wasanii/Artists
Popa Matumla
Raysa Art Designers

Timu ya Wahariri/Editorial Team
Rakesh Rajani
Godfrey Telli
Nyanda Shuli
Zainab Bakilana
Veena Gokhale
Richard Lucas

Mchapishaji/Publisher
© HakiElimu, 2005
PO Box 79401, Dar es Salaam, Tanzania
pub@hakielimu.org
www.hakielimu.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonukuliwa na kutuma nakala mbili za chapisho kwa HakiElimu.

Any part of this book may be reproduced for non commercial purposes, provided attribution is made to the source and two copies of the publication are sent to HakiElimu.

ISBN 9987-423-21-3

Utangulizi

Kwa kawaida malengo ya sera ni kutambua na kubainisha matatizo, au changamoto zinazochelewesha maendeleo ya wananchi, na jinsi zitakavyoshughulikiwa. Sera huchambua tatizo na kuonesha mikakati itakayofuatwa ili kupata suluhisho. Hivyo ni halali kabisa kwamba wadau wakuu, wa sera hizi ambao ni wananchi wa kawaida na walengwa hasa wa maendeleo ya nchi, wanapewa fursa sawa katika kubuni, kuandaa, kutekeleza na hatimaye kunufaika na sera za nchi. Kwa sababu zinawahusu moja kwa moja. Ni kwa misingi hii kwamba tunapofanya tathmini na kupima ufanisi wa hizi sera, vigezo vyetu viwe ni jinsi zinavyowaletea maendeleo. Maendeleo yasiyojali ustawi na hadhi ya wengi si maendeleo ya kweli na hayaashirii mustakabali mwema kwa taifa. Ili kuepusha shari huko mbele ya safari yapasa kujiuliza hizi sera zinabuniwa na nani na kwa maslahi ya nani.

Kijitabu hiki cha katuni ni cha nne katika mfululizo wa vijitabu kama hivi vinavyochapishwa na HakiElimu. Kinalenga mgongano unaojitokeza baina ya sera, mchakato mzima wa maendeleo na uhalisi wa mambo ulivyo kwa kutumia ucheshi. Shabaha ya katuni ni pamoja na kutanabahisha, kutoa changamoto, na kumulika vitendo vinavyokirihisha, ili tuvitafakari, tuvijadili na wenzetu na hatimaye tuhamasike na kuchukua hatua.

Ni ukweli usiopingika kwamba kati ya vigezo vya kupima kiwango cha maendeleo na ustaarabu katika jamii za kisasa ni uwezo wa kujicheka wenyewe. Katika kujicheka wenyewe, hujiona kama wenzetu wanavyotuona na hutathmini matendo na mwenendo wetu. Kwa mantiki hiyo basi wacha hizi katuni zizungumze nawe moja kwa moja. Zizungumze na jirani yako pamoja na familia yako. Huenda zikatuonyesha pale tunapopotoka, na pengine kutukumbusha wajibu wetu. Kwa mfano, Serikali, pamoja na watendaji wake, ambayo imechaguliwa na wananchi, inawajibika kwa nani? Na sisi raia wa kawaida tuna nafasi ipi katika mchakato mzima wa kuleta maendeleo? Tuiwajibisheje Serikali yetu ili itusaidie sisi? Mabadiliko sharti yaanze na sisi wenyewe, uwezo tunao wa kufanya hivyo.

Tafakari. Soma uelewe. Uliza maswali. Jadili na marafiki, familia na jirani. Zungumza na viongozi wa jumuia yako. Andika maoni na mapendekezo yako. Tuma kwa viongozi wako wa Wilaya, Kata na Kijiji. Na kama ukipenda, tuma nakala kwa Katibu Mkuu, Wizara husika (Anwani za Serikali zimeambatanishwa) na kwetu (HakiElimu, SLP 79401, Dar es Salaam). Au tuma barua fupi kwa mhariri wa gazeti au chombo chochote cha habari (Anwani za vyombo vya habari zimeambatanishwa).

Maoni yako ni muhimu. Nchi yako inahitaji kipaji chako, ubunifu wako, mawazo yako na kujitolea kwako ili kuifanya iwe nchi ya neema kama inavyostahili. Timiza wajibu wako.

Orodha na Anwani Za Wizara na Asasi Muhimu za Serikali

1	Mkurugenzi, Kurugenzi ya Habari na Mawasiliano, Ikulu.	S.L.P. 9120, Dar es Salaam.
2	Wizara ya Mendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.	S.L.P. 3448, Dar es Salaam
3	Wizara ya Elimu na Utamaduni	S.L.P. 9121, Dar es Salaam
4	Wizara ya Fedha	S.L.P. 9111, Dar es Salaam
5	Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, na Michezo	S.L.P. 3448, Dar es Salaam
6	Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu	S.L.P. 2645, Dar es Salaam
7	Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU)	S.L.P. 4865, Dar es Salaam
8	Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu	S.L.P. 9142, Dar es Salaam
9	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	S.L.P. 105081, Dar es Salaam
10	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma	S.L.P. 2483, Dar es Salaam
11	Mkurugenzi, Makamu wa Rais (AZISE)	S.L.P. 5380, Dar es Salaam
12	Mfuko wa Maendeleo wa Jamii (TASAF)	S.L.P. 9381, Dar es Salaam

Anwani za baadhi ya vyombo vya habari

Vyombo vya habari	Namba ya faksi	Namba ya simu	Sandukula la Posta
Alasiri	2773582	2700735/7	31042 DSM
BBC, Dsm		2127911/5	79545 DSM
Business Times	2150987, 2115025	2118378/9	71439 DSM
Clouds FM	2124649	2123919	31513 DSM
Daily News	2112881	2110595	9033 DSM
Daily Times	2150987	2118377/9	71439 DSM
DTV/CTN/ Ch.TEN	2113112	2116342	14678 DSM
East African radio	2775915	2775916	21122 DSM
Financial Times	2773583	2700735/7	31042 DSM
Ikulu	2113425	2116913	9120 DSM
ITV / Radio One	2775915	2775916	31042 DSM
Maelezo Hall	2113814	2122771	9142 DSM
Majira	2150987	2118377/9	71439 DSM
Mtanzania	2460030, 2123186	2461459	4793 DSM
Mwananchi	2450881, 2450886, 2450873	2450875-6/8	19754 DSM
Nipashe	2700146	2700735/7	31042 DSM
Radio Uhuru	2182369	2181700	9221 DSM
Rai	2460030, 2123186	2461459	4793 DSM
RTD	2865577	2860760/5, 2865564, 74	9191 DSM
Star TV/Radio Free Africa	028-2500713, 2136834	028-2503262, 2136834	1732 Mza; 6406 DSM
Sunday Observer	2773583	2700735/7	31042 DSM
Tanzania Daima	2126234	2126232	15261 DSM
The African	2460030, 2123186	2461459	4793 DSM
The Citizen	2450881, 2450886, 2450873	2450875-6/8	19754 DSM
The Express	2182659	2182665	20588 DSM
The Guardian	2773582	2700735/7	31042 DSM
TvT	2700011	2700466, 2700062, 32	31519 DSM
Victoria FM	028-2622944	028-2622091	1102 ARUSHA
Voice of Tabora		0744-261761	84 TABORA

Maoni yangu

My Opinion




© HakiElimu 2005

Sera, Mikakati Safi... Lakini Walengwa Je?


VIJANA WAKO WAMENIFUNGIA BIASHARA YANGU WANADAI MAZINGIRA MACHAFU. SHIKA HIZI UNISAIDIE, MZEE
HEEE HEEE -HEEH HII SI ND'O AJIRA, BWANA
KUMBUKA MVUNJA NCHI NI MWANANCHI
BW. AFYA KIJIJI
?
© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005


mmmm..... shule mimi basi.... na.....mwenzangu..... je?!...
?!
.....adhabu niliyopewa hainizuii kuendelea na shule
vijeba na wenye ƒedhwa mbona hawa wajibishwi?
nyumbani
ma.ha-kama
Shuleni
© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005

Sera, Mikakati Safi... Lakini Walengwa Je?


Awali...
Madeni nayamudu nita-endelea kukopa Sina wasiwasi!
MADENI
Baadaye...
JAMA NISAIDIENIII!!
MADENI
MZEE, VIPI TENA?
Sasa...
MADENI
Asante Mzee!
WAHISANI
SIJUI AMEPATA FUNDISHO?
© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005


ANA MAWAZO MAZURI YA MAENDELEO LAKINI SI MFUASI WA CHAMA CHETU!
UMENENA! NI KWELI, TUKIYAPOKEA TUTAKIPA SIFA CHAMA CHAO
SUALA LA MAENDELEO HALINA ITIKADI!
MKUTANO WA SERIKALI YA MTAA
© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005

Sera, Mikakati Safi... Lakini Walengwa Je?



Sera, Mikakati Safi... Lakini Walengwa Je?



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005


...HAO WANATAKA KUNIONA KIKAZI, WAACHE, WATASUBIRI TU! WE' DADA YANGU BWANA! ENHE, LETE STORI, NASIKIA ULIENDA NYUMBANI... MJOMBA ANASEMAJE?..
TAFADHALI MAMBO YA 'KINDUGU' USILETE OFISINI!
utawala
HUYU BOSI TULI-SOMA PAMOJA 'MIDO-SKULI'. NIINGIE TUPIGE STORI ZA SHULE
© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005


Wakati wa kampeni...
NINA MIEZI MIWILI YA KUBEMBELEZA KURA
...nitawaletea matrekta kila mkulima, nyumba, mabomba, barabara...
© HakiElimu 2005
Baada ya uchaguzi...
GAZETI LIDAKU
MHESHIMIWA, ZILE AHADI VIPI?
UBUNGE
...SASA ZAMU YENU KUPIGA MAGOTI KWA MLAKA MITANO!



© HakiElimu 2005

Sera, Mikakati Safi... Lakini Walengwa Je?



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005

Sera, Mikakati Safi... Lakini Walengwa Je?



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005


ANGALIA VITOTO! ALMANUSRA VIGONGWE. SIJUI KWANINI VINAPENDA KUCHEZA BARABARANI?
HUYO ALIYEWAKOSA, NDIYE HUYO-HUYO ALIYEPORA KIWANJA CHAO CHA KUCHEZEA!
HOLA!
MT. USWAHILINI
KWANI MAMLAKA HUSIKA ZIKO LIKIZO?
© HakiElimu 2005
kamtuego.com



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005


NAFANYA UTAFITI JUU YA UKUBWA WA TATIZO LA RUSHWA, NAAMINI OFISI YAKO ITAKUWA NI MSAADA MKUBWA
AH, SANA! TAARIFA ZOTE ZIPO! LAKINI 'MGOGORO' WA KUYA-CHAMBUA MAFAILI HUSIKA... ITABIDI U... YAANI U...NANIHI NADHANI NAELEWEKA
MTAFITI
!?
kamtu@go.com
© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005


TUNASHUKURU NA UCHAGUZI WA MWAKA HUU MAENDELEO KIDOGO TUMEPATA. SI UNA-ONA MWENYEWE
KWELI! TUMEAMBULIA TENA KHANGA! HIZI WALIZOTUGAWIA MIAKA MITANO ILIYOPITA TAYARI ZILIKUWA HAZITAZAMIKI KWA KUCHAKAA!
MASIKINI! ND'O KINACHO-WAPONZA!
kamtu@go.com
© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005




© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005



© HakiElimu 2005


HALI SHWARI KABISA HAPA, MHESHIMIWA, HATUNA MATATIZO YOYOTE
NDIO INAVYO-TAKIWA. HONGERA SANA!..
LAKINI NGOJA TUWASIKILIZE NA WANANCHI
MNAMSIKIA KIONGOZI WETU JAMANI?... HATUNA MAJI HAPA!..
USIMSIKILIZE HUYO!
ZAHANATI HAINA DAWA!
Pembejeo!
MAJI TUNA-KUNYWA NA NGOMBE!
!?
© HakiElimu 2005
kamtuego.com



© HakiElimu 2005

Sera, Mikakati Safi... Lakini Walengwa Je?


SHULE WANAYOFUNDISHA IMEKARABATIWA VIZURI LAKINI HALI YA WALIMU WENYEWE JE?
BWANA WEEH!
SHULE
Majengo yame-boreshwa. Maslahi je?
© HakiElimu 2005

Kuhusu kitabu hiki

Hiki ni kitabu cha nne katika muendelezo wa vijitabu vya katuni vya HakiElimu. Katuni hizi zinatuelimisha na kutuburudisha lakini la muhimu zaidi zinatupa changamoto na kutuhamasisha tutoe mchango wetu katika masuala ya maendeleo ya taifa letu kwa kadri ya uwezo wetu.

Wahusika katika katuni wanaonekana watundu au wakorofi. Wakati mwingine wanachekesha lakini maneno yao yanabeba ujumbe mzito unaogusa hisia zetu. Mabadiliko ambayo yataleta maendeleo, katika nyanja za elimu, haki za binadamu au ustawi wa jamii, yatapatikana kwa juhudi zetu wenyewe, hasa kama sisi wananchi wenye mwamko tutayajadili masuala hayo na kuchukua hatua. Kijitabu hiki kinatumia njia ya ucheshi, kuchangia katika shughuli hii muhimu.

About this book

This Cartoon Booklet, fourth in the series produced by HakiElimu, focuses on the gaps between policy and practice. It highlights contradictions in development, using humor. The aim of these cartoons is not to merely criticize, but to appreciate, amuse, challenge and above all, to stimulate thought, debate and action.



The characters in the cartoons are cheeky and funny, but they carry messages which are disturbingly serious. Transformation of our society, be it in the field of education, human rights, governance or social welfare, will be possible only if informed citizens take action. This booklet is a light hearted contribution to that serious task.

HakiElimu inafanya kazi kuleta usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika Elimu, kwa kuziwezesha jamii kubadilisha mifumo ya uendeshaji wa shule, kuwa na ushawishi katika utayarishaji wa sera, kuhamasisha majadiliano ya kibunifu ya umma kwa lengo la kujiunga pamoja kuleta mabadiliko, kuendesha tafiti zinazohoji na kuchambua mambo kwa kina, kuendesha kampeni za utetezi na kushirikiana na wabia wengine ili kufikia malengo ya pamoja na kupigania haki ya jamii.

HakiElimu works to realize equity, quality, human rights and democracy in education by facilitating communities to transform schools and influence policy making, stimulating imaginative public dialogue and organizing for change, conducting critical research, policy analysis and advocacy and collaborating with partners to advance common interests and social justice.

S.L.P 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org
Simu: +255 22 2151852/3 • Faksi: +255 22 2152449